
Majukumu ya Wanafunzi Katika Utawala wa Shule



Kwanini wanafunzi washiriki katika utawala?

Baadhi ya watu wanafikiri kwamba watoto wanatakiwa kuwepo shuleni kwa ajili ya kusoma tu na hawapaswi kushiriki katika utawala. Wanasema kwamba watoto hawajakomaa kiakili kiasi cha kuweza kuhusishwa katika kufanya maamuzi muhimu. Lakini kuna sababu nzuri za wanafunzi kushiriki katika maamuzi. Baadhi ya sababu hizo ni:

- Wanafunzi wana utambuzi. Wanafunzi wanafahamu kinachoendelea shuleni, na wanauwezo wa kuchangia mawazo kwa vitendo na kuleta mabadiliko. Mathalan, wanaweza kusema iwapo rasilimali za shule zimetumika vyema, ni walimu wapi wanaowahi darasani, na nini kinaweza kufanyika kuwezesha shule kuwa mahali bora.
- Watoto wanajifunza kwa vitendo. Kwa kushiriki katika kutoa maamuzi, watoto wanapata ujuzi katika maisha na jinsi ya kulinganisha mambo mbalimbali, kutetea hoja, na kutoa mapendekezo. Wanafunzi watajifunza jinsi demokrasia inavyofanya kazi, na kutumia ujuzi huo nyumbani na katika jumuiya.
- Ushiriki ni umiliki. Wanafunzi walioshirikishwa katika kubuni jambo, wana nafasi kubwa ya kulielewa, kuona umuhimu wake na kujitolea. Kwa mfano, sheria na taratibu zilizobuniwa na kuongozwa kwa ushiriki wa wanafunzi zina nafasi kubwa ya kukubalika na kuheshimika.
- Ushiriki ni haki. Wanafunzi ni binadamu kamili na wana haki za kimsingi. Mkataba wa kimataifa wa Haki za Watoto, ambao Tanzania imeridhia, unatambua haki ya watoto kushiriki katika masuala yote yanayowahusu (Kifungu. 12-15). Mpango wa serikali wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) pia unatambua na kuelekeza jinsi wanafunzi watakavyoshiriki.

MMEM inasemaje kuhusu Wanafunzi na Utawala?

MMEM inatambua umuhimu wa wanafunzi kushiriki katika utawala wa shule kupitia Baraza la Wanafunzi na Baraza la Shule. Kiambatanisho cha MMEM kuhusu ushiriki wa wanafunzi kimenukuliwa (angalia kisanduku).

Kwa mujibu wa MMEM, wanafunzi wanaoshiriki katika utawala wana majukumu yafuatayo:

- Kuwakilisha maoni na mahitaji ya wanafunzi wote, wakiwemo wale walioachwa pembezoni na wenye mahitaji maalum, katika utawala wa shule na katika kufanya maamuzi na ndani ya kamati za shule.
- Kuunda na kusimamia mipango ya shule na matumizi ya fedha.
- Kusambaza taarifa kati ya shule/ uongozi wa kijiji na wanafunzi

Mwongozo huu katika sera unawapa wanafunzi haki ya kusikilizwa na fursa ya kuboresha shule. Wanafunzi pia watahitaji kuwajibika. Wanahitaji kufikiri, kutenda haki, kuheshimu na kuwajumuisha wale ambao kwa kawaida sauti zao hazisikiki. Mwongozo unaeleza kuwa mwalimu, awe amechaguliwa na wanafunzi, kuwaongoza kiuraghabishi. Kamati za shule zinapaswa kuhakikisha kuwa vipengele vyote vya MMEM, kikiwemo cha ushiriki wa wanafunzi, vinatekelezwa ipasavyo.



Kiambatanisho cha 6
Muhtasari wa Utaratibu kwa Ushiriki wa Wanafunzi katika Utawala wa Shule



Wanafunzi wawili kutoka katika kila mkondo (mvulana 1, msichana 1) watachaguliwa na wenzao kuwa wajumbe wa Baraza la wanafunzi. (Uchaguzi utaanzia darasa la 3, ikiwa wanafunzi wa darasa la 1 na 2 watachukuliwa kuwa ni wadogo mno.) Kwa nyongozea, nafasi 2-4 za "viti maalum" vya ziada zinaweza kutolewa kwa watoto wenye ulemavu au wenye mahitaji maalum.

Jukumu la wanafunzi litakuwa a) Kuwakilisha matakwa ya wanafunzi wenzao katika Baraza la Wanafunzi b) Kupeana taarifa na wenzao darasani zinazotoka katika Baraza la Wanafunzi. Hii inahitaji wawakilishi wa wanafunzi kuwajibika kwa kupitia mkutano rasmi wa darasa unaoitishwa kwa madhumuni haya mara moja kwa mwezi.

Mkutano wa wawakilishi wote wa wanafunzi utaunda Baraza la Wanafunzi. Baraza litakuwa na uongozi wake uliochaguliwa kidemokrasia ambao utajumuisha mwenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu na wawakilishi wawili katika kamati ya shule. Nafasi nyingine za uongozi pia zinaweza kuundwa kama itakavyotakiwa na Baraza la Wanafunzi. Kwa kawaida Baraza la Wanafunzi litakutana mara moja kwa mwezi na zaidi ya hapo kama ni muhimu.

Wawakilishi wa wanafunzi katika kamati ya shule watapokea maagizo yao na watawajibika kwa Baraza la Wanafunzi. Wawakilishi/viongozi wote wa wanafunzi watatumikia kwa kipindi cha mwaka mmoja na wanaweza kuchaguliwa tena.

Mwalimu/mshauri mkuu wa wanafunzi atahudhuria mkutano wa Baraza la Wanafunzi kama mtazamaji. Kazi ya mtu huyu itakuwa a) kuwezesha, kuendeleza uwezo wa wanafunzi na b) kuwa kama nguzo ya kupitishia taarifa kati ya wanafunzi na walimu/utawala wa shule (Viongozi wa Baraza la Wanafunzi pia watawasiliana wenyewe na uongozi wa shule). Mwalimu/mshauri huyu atachaguliwa kwa uangalifu, hasa na wanafunzi wenyewe ili kuhakikisha anaweza kufanya kazi ya uwezeshaji na kuepuka kuhodhi au kuitawala mikutano ya Baraza la wanafunzi.

Kwa nyongeza muhtasari wa a) Baraza la Wanafunzi, b) walimu/wafanyakazi na c) mikutano ya kamati ya shule itawasilishwa na masuala muhimu yatajadiliwa katika mkutano wa kila mwezi wa Baraza la Shule. Baraza hili halipaswi kutawaliwa na Mwalimu Mkuu/ walimu au kuwa sehemu ya kutolea matangazo, badala yake kuwa fursa ya kupeana taarifa na kujadiliana kuhusu masuala muhimu miongoni mwa jumuiya nzima ya shule. Wazazi ambao ni wajumbe wa kamati ya shule wataalikwa kushiriki katika Baraza. Baraza ni lazima liandaliwe na kuendeshwa kwa ushirikiano wa Mwalimu Mkuu na Mwenyekiti wa Baraza la Wanafunzi.

Mchakato mzima ni lazima uzingatie kanuni zenye heshima, shirikishi, zenye uwazi, uaminifu na maadili mengine yanayolingana na shule zinazowajali watoto na zinazoheshimu haki.

Ni dhahiri mfumo wa kidemokrasia ulioelezwa hapo juu unawakilisha mkengeuko mkubwa kutoka katika utendaji wa sasa katika ngazi ya shule. Mwongozo na taratibu za wazi zitahitaji kuundwa na mkakati utengenezwe kukuza dhana katika ngazi zote. Mabadiliko yatachukua muda, na yatahitaji kujengewa uwezo, ikiwa ni pamoja na kunukuu uzoefu uliopatikana, kubadilishana uzoefu wa utendaji mzuri, n.k. Mpango madhubuti wa jinsi ya kufanya haya utahitaji kutengenezwa, na utakuwa ni sehemu ya mpango katika programu ya kujenga uwezo wa kamati ya shule.

Imetafsiriwa na HakiElimu kutoka kitabu cha: Uimarishaji wa taratibu za kitaasisi, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), Agosti 3, 2001

Nitafuatiliaje?

Kila mtu ana haki ya kupata habari, na kila mmoja ana haki ya kufahamu juu ya ushiriki wa wanafunzi katika MMEM. Kwa kuwa sasa unafahamu kwamba MMEM inasema nini kuhusu ushiriki wa wanafunzi, unaweza kuona kama haya yanafanyika katika jumuiya yako, uliza maswali kama hayo hayafanyiki na utoe mawazo yenye kujenga ya kufanya mambo yawe bora zaidi. Kwa mfano, unaweza kuuliza kama Baraza la Wanafunzi linakutana katika shule yako, na jinsi gani washiriki walivyochaguliwa kidemokrasia na wanafunzi wenzao.

Una haki ya kuuliza maswali na kupata majibu fasaha. Kwa mujibu wa mabadiliko ya Serikali, haikubaliki tena kwa kiongozi kutoa amri tu bila kuwasikiliza watu. Ni dhahiri mabadiliko huchukua muda, na hatutegemei kwamba kila kitu kitakuwa timilifu mara moja. Hata hivyo, una haki ya kuona maendeleo yakitokea.

Unaweza kupata habari kutoka kwa mwalimu mkuu, Afisa Elimu wa Wilaya, Diwani au Mbunge wako. Unaweza kuomba taarifa kutoka Mkutano wa Kijiji/Mtaa au vikao vya Halmashauri. Unaweza pia kuuliza Asasi Zisizo za Serikali (AZISE) katika eneo lako.

hakielimu

SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (022) 2151852 / 3 • Faksi (022) 2152449 • info@ hakielimu.org • www.hakielimu.org